Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

LA MTANDAONI | JANUARI 2022 - DESEMBA 2022

# MATUKIO MUHIMU YAKUKUMBUKWA KUHUSU NSSF MWAKA 2022




## YALIYOMO:


- WAZIRI NDALICHAKO ALIVYOGUSWA HUDUMA ZA NSSF
- NSSF ILIVYOFANYA MATENDO YA HURUMA, YATOA MSAADA WA VIFAA TIBA


Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii **(NSSF)** ulianzishwa chini ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii sura ya 50 marejeo ya mwaka 2018 kwa lengo la kutoa huduma ya Hifadhi ya Jamii kwa wafanyakazi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Mfuko una majukumu yafuatayo kwa mujibu wa sheria ambayo ni **kuandikisha wanachama** kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi, **kukusanya michango, kuweza** na **kulipa mafao.**

NSSF inakuletea matukio muhimu ya kukumbukwa yaliyotokea kuanzia mwezi Januari mpaka Desemba 2022 ambayo yalikuwa chachu ya mafanikio kwa Mfuko, wanachama, wadau pamoja na sekta nzima ya hifadhi ya jamii nchini Tanzania.

@NssfTanzania

**TUNAJENGA MAISHA YAKO YA SASA NA BAADAYE**




*Mhe. Profesa Joyce Ndalichako*
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*

# WAZIRI NDALICHAKO ALIVYOGUSWA HUDUMA ZA NSSF

**Na MWANDISHI WETU**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Profesa Joyce Ndalichako (Mb) alifanya ziara ya kutembelea Makao Makuu ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) jijini Dar es Salaam, tarehe 27 Januari, 2022 na kushuhudia huduma zinazotolewa na Mfuko kwa wanachama na wadau wake. Hiyo ilikuwa ni ziara yake ya kwanza kwa Profesa Ndalichako kutembelea NSSF baada ya kuteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongoza Wizara hiyo ambayo NSSF ni miongoni mwa taasisi zilizo chini yake.






# NSSF ILIVYOFANYA MATENDO YA HURUMA, YATOA MSAADA WA VIFAA TIBA

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ulitoa msaada wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Zanzibar, ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambavyo ni vitanda vya kujifungulia pamoja na mashine za kupima shinikizo la damu ambavyo vitasaidia kuokoa maisha ya wagonjwa wanaopata huduma katika hospitali hiyo. Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko, Masha Mshomba, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Bi. Lulu Mengele pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa NSSF walikabidhi vifaa hivyo kwa uongozi wa hospitali hiyo mnano tarehe 4 Machi, 2022.




Baadhi ya wafanyakazi wa NSSF wakikabidhi msaada wa vifaa tiba katika hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar

# SABABU ZA NSSF KUSHIRIKI UZINDUZI WA SGR

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulishiriki katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika mradi wa SGR Makutupora mkoani Tabora, uliofanyika tarehe 13 Aprili, 2022. Tokea mradi huo ulipoanza, Mfuko umekuwa mdau mkubwa kwa kuweza kukusanya kila mwezi zaidi ya shilingi bilioni moja kutoka kwenye mradi huo.



*Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma Mheshimiwa Jerry Silaa (Mb) watatu kulia, akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watendaji wa NSSF mara baada ya kutembelea banda la NSSF katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR mkoani Tabora. Wa tatu kushoto ni Meneja wa NSSF Mkoani Tabora, Paulo Shimo, (wa pili kulia) ni Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma NSSF, Lulu Mengele*


# NAMNA NSSF ILIVYOSHIRIKI SHEREHE ZA MEI MOSI

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulishiriki sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) zilizofanyika jijini Dodoma Kitaifa, ambapo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa mgeni rasmi. Kabla ya sherehe hizo, Mfuko ulishirikia Maonesho ya Wiki ya Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) yaliyofanyika katika Viwanja vya Jakaya Kikwete Convention Centre jijini Dodoma. NSSF ilitumia maonesho hayo kwa lengo la kutoa elimu na kuandikisha wanachama wapya, ambapo kupitia maonesho hayo Mfuko uliibuka mshindi katika kundi la watoa elimu.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba akipokea Tuzo ya kundi la Watoa Elimu bora kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Dkt. Profesa Joyce Ndalichako katika maonesho ya OSHA yaliyofanyika jijini Dodoma*

# `BOOM VIBES' NA NSSF YATIKISA, MAMIA YA WANAVYUO WAJIUNGA NA NSSF



**Na MWANDISHI WETU**

Ni kampeni iliyoanzishwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kupewa jina la `*Boom Vibes'* na NSSF ambapo kupitia kampeni hiyo Mfuko ulifanikiwa kuwafikia baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali nchini, kwa lengo la kuwapa elimu ya hifadhi ya jamii ambapo mamia ya wanavyuo hao waliamua kujiunga na kujiwekea akiba kwa ajili ya maisha yao ya sasa na baadaye.



*Baadhi ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao pia ni wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Katiba na Sheria wakiwa katika picha ya pamoja na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dodoma waliofikiwa na NSSF wakati wa Kampeni ya `Boom Vibes' na NSSF*

# NSSF ILIVYOWAJENGEA UWEZO WAAJIRI WA SEKTA BINAFSI

Katika kuhakikisha elimu ya hifadhi ya jamii inapata uelewa mkubwa, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uliendesha mafunzo kwa waajiri wa sekta binafsi kwa lengo la kuwafahamisha kuhusu huduma za Mfuko zikiwemo matumizi ya TEHAMA hususan huduma za taarifa binafsi kwa mwajiri 'Employer Portal' mifumo ambayo inamuwezesha mwajiri kujihudumia bila ya kufika katika ofisi za NSSF.



*Baadhi ya waajiri wa sekta binafsi wakifuatilia mafunzo yaliyotolewa na NSSF kwa waajiri. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwenye mikoa mbalimbali kwa lengo la kuwahamasisha kuhusu huduma za Mfuko zikiwemo za matumizi ya TEHAMA.*

# WANANCHI WALIVYOFIKIWA NA HUDUMA ZA NSSF KATIKA MAONESHO YA SABASABA

Wananchi walifikiwa na huduma zitolewazo na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wakati wa Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara maarufu kama 'Sabasaba' yaliyofanyika Viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, ambapo kupitia maonesho hayo Mfuko ulitoa elimu ya hifadhi ya jamii, kutatua kero za wanachama pamoja na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji.




*Wanachama na wadau wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wakipata huduma mbalimbali kutoka kwa wafanyakazi wa NSSF walipotembelea banda namba 13 wakati wa Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara maarufu Sabasaba*



## WAZIRI NDALICHAKO ALIVYOTATUA KERO ZA WASTAAFU

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulishiriki katika mkutano wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Profesa Joyce Ndalichako, ambaye mwezi Julai 2022 kwa nyakati tofauti alikutana na wastaafu wa Mkoa wa Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza kwa lengo la kusikiliza changamoto zinazohusiana na ulipwaji wa mafao kwa wastaafu wa Mifuko ya NSSF na PSSSF.





*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Dkt. Profesa Joyce Ndalichako akiwasikiliza wastaafu na kutatua kero zao.*

# NSSF ILIVYOTIKISA NANENANE, YAFIKISHA ELIMU NA KUTATUA KERO




**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulifanikiwa kufikisha elimu ya hifadhi ya jamii kwa wananchi wakiwemo wakulima walioshiriki Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika katika Mkoa wa Mbeya, Dodoma, Simiyu, Tabora na Lindi, ambapo kupitia maonesho hayo NSSF iliweza kutoa elimu na kuandikisha wanachama wapya.













## `*VIBE*' LA NSSF WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ulishiriki kimkakati katika Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyofanyika mwezi Oktoba 2022 ikiwa na kauli mbiu isemayo Huduma Bora, Kipaumbele Chetu; ambapo kupitia wiki hiyo kero mbalimbali za wanachama ziliweza kutatuliwa.

Katika maadhimisho hayo ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, iliadhimishwa katika ofisi za NSSF nchi nzima.






*Katika picha ni matukio mbalimbali wakati Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba aliposhiriki uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja 2022 yaliyofanyika jengo la Mafao House jijini Dar es Salaam*

# NSSF ILIVYOSHIRIKI MKUTANO WA RAIS DKT. SAMIA NA MABALOZI

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba alihudhuria katika mkutano wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabalozi wa Tanzania uliofanyika Hotel Verde, Zanzibar. Katika mkutano huo Mshomba akiwa ni mjadili mada alipata nafasi ya kuzungumzia fursa za uwekezaji zilizopo NSSF.




*Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (wa tatu kushoto) akiwa katika Mkutano wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabalozi, uliofanyika Hotel Verde, Zanzibar.*

# NSSF ILIVYOSHIRIKI MASHINDANO YA SHIMMUTA

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulikuwa ni miongoni mwa Mashirika ya Umma yaliyoshiriki katika mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika katika viwanja vya Mkwakwani Mkoani Tanga. Aidha, Mfuko pamoja na kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuweka na kulipa mafao, vilevile umekuwa ukishiriki katika masuala mbalimbali ya kijamii ikiwemo michezo ili kuimarisha afya za wafanyakazi mahali pa kazi.




*Baadhi ya wafanyakazi wa NSSF walioshiriki mashindano ya SHIMMUTA 2022 wakiwa katika maandamano ya pamoja wakati wa uzinduzi wa mashindano hayo yaliyofanyika katika uwanja wa Mkwakwani, jijini Tanga.*

# SABABU ZA NSSF KUSHIRIKI SIKU YA UKIMWI DUNIANI



Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulishiriki katika maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Ilulu Mkoani Lindi, ambapo NSSF ilishiriki kutoa huduma, kuandikisha wanachama wapya na pia ulihamasisha jamii kujikinga na maambukizi ya VVU/Ukimwi ili kulinda nguvu kazi. Hiyo inaendana sambasamba na Sera ya UKIMWI mahali pa kazi.

# BODI YA NSSF YAKAGUA MAENEO YANAYO -MILIKIWA NA NSSF



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya NSSF, Balozi Ali Idi Siwa, akiwa na baadhi ya wajumbe wa Bodi na wafanyakazi wa NSSF walifanya ziara ya kukagua maeneo yanayomilikiwa na NSSF, jijini Dar es Salaam na Mkoani Morogoro.

BOARD OF TRUSTEES
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND
NSSF

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF